





Mkanda wa video hiyo yenye takriban dakika 39 na sekunde 34, unamuonesha pia Miss Ilala namba tatu mwaka 2005, Jacqueline Patrick akishiriki kikamilifu kwenye tukio hilo la kudhalilisha.

Kwa mujibu wa video hiyo, Jacqueline havui nguo, badala yake ameonekana kushiriki kama mmoja wa waratibu wa shughuli nzima huku akiwapiga picha akina mama waliokuwa wakicheza uchi.

Hali halisi ya mkanda huo ni kuwa, umerikodiwa katika hoteli moja ya kifahari jijini Dar es Salaam huku wahudumu wa kiume wakionekana kuzunguka wakiwahudumia wateja.

Mbali na hao, pia kuna wanawake watatu wenye asili ya Kiarabu ambao nao hawavui nguo, isipokuwa wanaonekana kama ni miongoni mwa walioiwezesha shughuli hiyo.

Kwa mujibu wa mleta habari wetu, muwezeshaji wa video hiyo ni mwanamke aliyetajwa kwa jina moja la Nancy ambaye naye ni mdau wa ‘umisi’ hapa nchini na aliurekodi ili kwenda kuuza China.

“Kila kitu kiliandaliwa na Nancy kisha Jacqueline alishiriki katika kuwatafuta wanawake waliocheza video hii,” alisema mleta habari wetu bila kufafanua jina la pili la huyo Nancy.

Aidha, mtoa habari huyo aliwataja kwa majina moja moja, wahusika wakuu wawili katika zoezi la kucheza uchi kwenye mkanda huo kuwa ni Mwajabu na Kashinde, wakazi Kinondoni Mkwajuni, Dar es Salaam.

Alisema, waliocheza uchi waliahidiwa kulipwa ujira wa shilingi 100,000 lakini wakapewa shilingi 50,000 kama kianzio.



“Mkanda mzima unajumuisha wanawake karibu 20, wanaume wapatao saba ambao ni wahudumu wa hoteli, ingawa waliokuwa wanavua nguo ni wanawake wanne, lakini mimi nawajua wawili, Mwajabu na Kashinde,” alisema.

Gazeti hili, liliwatafuta Mwajabu na Kashinde ili kujua sababu ya wao kukubali kucheza video hiyo wakiwa uchi. Maelezo yao tutayachapisha katika gazeti hili wiki ijayo.

**Ndugu msomaji huu ni udhalilishaji na tunalaani vikali vitendo hivi. Habari hii itaendelea ili kufichua mengi yaliyofichika. Ombi linatolewa kwa wasomaji wote wa mtandao huu wenye habari zaidi kuhusu mtandao huu kuwasiliana nasi ili kufichua maovu haya- Mhariri.**

Dear Guest you have enter our site without being Registered. We recommend to register to view more...
"Mgeni wetu unatakiwa **Kuregista** kupata